**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24 NA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24

**MACHI 13, 2023**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24 NA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24**

## UTANGULIZI

~~1.~~ ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 pamoja na Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24.

~~2.~~ ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini katika kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango, Mhe. Hamad H. Chande, Katibu Mkuu Dr. Natu El-Maamry Mwamba pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa uchapaji kazi wao na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya shughuli za Serikali.

3. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu: Sehemu ya Kwanza ni Tathmini ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi; Sehemu ya Pili ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 na Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/24; na Sehemu ya Tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023 na Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24.

## SEHEMU YA KWANZA

## TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI

4. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kutokana na Changamoto za kukabiliana na Tatizo la Ajira, kukuza uchumi na kuhakikisha Taifa letu linajenga Uchumi shindani na himilivu, serekali ya Awamu ya sita katika mwaka wa fedha 2022/2023 iliamua kuhakikisha inawekeza nguvu kubwa kwenye sekta za uzalishaji ambazo matokeo yake yatakua ya muda mrefu na uwekezaji utakua mkubwa. Utakumbuka athari za COVID -19 na mzozo wa Urusi na Ukraine imebadilisha mifumo na mitazamo ya chumi zote duniani iliyoathiri mifumo ya uzalishaji, usafirishaji, uuzaji na ununuzi. Serekali iliamua kuanza safari ya kuhakikisha tunajenga uchumi shindani na himilivu. Ili kufikia lengo hilo, Serkali iliamua kuwekeza kwenye eneo la kilimo, mifugo, uvuvi na nishati. Hatua hizi zimechangia kuleta matokeo yafuatayo: Kuimarika kwa sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi na nishati; kuimarika kwa miundombinu ya huduma za kiuchumi ikiwemo barabara na madaraja, reli,

usafiri na usafirishaji wa majini na angani na TEHAMA; kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na biashara, hivyo kuvutia ushiriki wa sekta binafsi na ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi; na kuimarika kwa rasilimali watu na huduma za jamii ikiwemo afya, elimu, maji na ardhi na makazi hivyo kuimarika kwa ustawi wa wananchi na kupungua kwa kiwango cha umaskini. Mwelekeo huu utaendelea katika mpango na bajeti ijayo.

5. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Uchumi wa Tanzania umeendelea kuwa imara licha ya kukumbwa na athari za UVIKO-19 na vita inavyoendelea baina ya Urusi na Ukraine, mambo ambayo yameathiri uchumi wa dunia kwa ujumla. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2022 uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 22.5 Desemba 2022 ikilinganishwa na asilimia 10 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,177.2 Desemba 2022 iliyotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.7. Kiwango hiki ni ndani ya lengo la nchi na lengo la kimataifa la akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa kwa miezi isiyopungua minne (4). Aidha hadi Desemba 2022, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 74,637.91 kufuatia kuendelea kupokelewa kwa fedha za mikopo zinazotumika kwenye utekelezaji wa miradi mikubwa ya kielelezo ndani ya nchi yetu. Mfumuko wa bei nchini ulifikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2021. Kiwango hiki kipo ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya Jumuiya ya Africa Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) vya asilimia 5.0 na asilimia 8.0 mtawalia.

6. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Hali ya mfumuko wa bei inayoendelea imechangiwa na:

(i) Kuongezeka kwa bei ya bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje ya nchi hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea, ngano na malighafi za viwandani ambazo zilipelekea gharama za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la ndani kuongezeka hususan bei za bidhaa zilizozalishwa na kusambazwa kabla ya hatua ya Serikali kutoa ruzuku;

(ii) Kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya ndani kutokana na mabadiliko ya tabianchi, hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli ambayo hayakupata mvua na sehemu nyingine hazikupata mvua za kutosha katika mwaka rejea wa taarifa hii;

(iii) Kuongezeka kwa mahitaji ya chakula kutoka nchi jirani hususan ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika ambazo ziliathiriwa na kupanda kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji na mabadiliko ya tabianchi.

(iv) Kuongezeka kwa fedha kwenye mzunguko wa uchumi kutokana na kasi ya utekelezaji wa miradi, ulipaji wa madeni kwa watoa huduma, wazabuni, makandarasi, watumishi wa umma na ajira mpya hivyo kuongeza uhitaji wa bidhaa unaopunguza uwiano wa mahitaji na upatikanaji wa bidhaa.

7. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kudhibiti mfumuko wa bei katika soko la ndani, ikiwemo:

(i) Kuchukua hatua mahsusi za kutoa ruzuku ya mafuta (Fuel) na mbolea;

(ii) Kuchochea na kuhamasisha uzalishaji na usambazaji wa mazao ya muda mfupi, hususan maharage, mbogamboga, mbegu za mafuta ya alizeti na pamba na usambazaji wa tani 14,748.13 za mahindi kutokea NFRA katika maeneo yenye upungufu wa chakula katika Halmashauri 47 na kuuzwa kwa bei nafuu;

(iii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa sera za bajeti na fedha hususan kutoa misamaha ya kodi, ushuru na tozo katika baadhi ya bidhaa ili kupunguza bei za bidhaa hizo;

(iv) Kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia ili kufungamanisha na mahitaji ya soko la ndani; na

(v) Kuongeza na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua katika uzalishaji wa mbegu, mazao ya chakula na biashara sambamba na kupunguza uagizaji wa mazao ya kilimo ambayo yana fursa ya kuyazalisha nchini.

8. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** mwenendo mzuri wa viashiria vya uchumi jumla ni matokeo ya jitihada mbalimbali zilizotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya usimamizi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jitihada hizo ni pamoja na: Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara hususan utashi wa kisiasa wa kufanya majadiliano na wawekezaji wa ndani na nje; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye mchango mkubwa na matokeo chanya katika ukuaji wa uchumi; kuendelea kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo*;* usimamizi bora wa masuala ya sera za nchi kiujumla; na utekelezaji madhubuti wa programu ya *Extended Credit Facility* (ECF) inayosimamiwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Programu ya *Development Policy Operation* (DPO) inayoratibiwa na Benki ya Dunia katika mkakati wa kufufua na kuchochea kuimarika kwa uchumi. Maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa hali ya uchumi yameainishwa katika **Sura ya Kwanza ya Kiambatisho cha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24.**

## SEHEMU YA PILI

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23 NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2023/24

### A. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23

9. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika mwaka 2022/23, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 15,006.0, sawa na asilimia 36.2 ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 12,306.9 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,699.1 ni fedha za nje. Hadi Januari 2023, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ni shilingi bilioni 8,636.7, ambapo shilingi bilioni 7,047.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1,588.9 ni fedha za nje.

10. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** kiasi kikubwa cha fedha kinachotolewa na Serikali kinaelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ina manufaa mapana katika uchumi na kuleta tija kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya msingi ya kiuchumi, mazingira ya biashara na uwekezaji, huduma za jamii, kuimarisha hali ya demokrasia, haki na utawala bora nchini.

11. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kama ifuatavyo:

**A; Sekta za Uzalishaji**

(i) **Kilimo:** Kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji; kuimarisha huduma za ugani, vyuo vya mafunzo ya kilimo na vituo vya mafunzo ya wakulima; kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora na mbolea ya ruzuku ambapo jumla ya tani 297,599.18 za mbolea za ruzuku zilisambazwa katika maeneo mbalimbali nchini; na kubainishwa mashamba makubwa (block farms) yenye ukubwa wa ekari 183,012 kwa ajili ya vijana katika mikoa ya Mbeya, Dodoma, Kagera na Kigoma ambapo vijana 812 wamedahiliwa kwa ajili ya kupewa mafunzo katika vyuo vya kilimo kabla ya kupewa ardhi ya kilimo. kukamilika kwa ujenzi wa vihenge vya kisasa vya kuhifadhi mazao katika vituo vya Babati na Sumbawanga; kukamilika kwa maghala 10 ya kuhifadhi nafaka ili kupunguza sumukuvu; kukamilika kwa ujenzi wa kilometa 85.6 za barabara za vijijini katika maeneo yanayozalisha chai, kahawa na mazao ya mbogamboga na matunda; kugawa pikipiki 3,500 kwa maafisa ugani katika mikoa 15; na kukamilika kwa kituo cha udhibiti wa magonjwa ya mimea kibailojia. Jumla ya shilingi bilioni 222.5zimetumika katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023;

Hatua zingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuongeza fedha za uzalishaji wa mbegu utoaji wa Ruzuku ya mbolea na Uwekezaji wa umwagiliaji uanzishaji wa Mashamba ya Blockfarm kwa ajili ya vijana na kukabiliana na tatizo la Ajira. Miradi yote hii imeanza kutekelezwa na matokeo yake kwenye uchumi tutayaona baada ya miaka 3 kwakua mwelekeo wa huu mpya wa uwekezaji kujenga uchumi shindani na himilivu ni ya muda mrefu. Kwa mfano, bajeti ya kilimo iliongezeka kutoka bilioni 294 mpaka bilioni 954 na tutaendelea kuongeza katika Bajeti za miaka ijayo ukiwa ni uwekezaji wa Serekali na hasa maeneo ya Ugani, Umwagiliaji uzalishaji wa mbegu na baada ya miaka 3 miradi hii tulioanza kujenga mwaka huu ya hekta 90,000 na usanifu wa mabonde ya Ziwa viktoria ,Lake Tanganyika, Bonde la songwe, Mto ruhuhu, Ruvuma basin ,Manonga, Wembere, Malagalasi na Rufiji Basin lengo kuu la serekali ni kuhakikisha inapofika mwaka 2030 asilimia 50 ya shughuli za kilimo zinafanyika kwa umwagiliaji. Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lazima lijitegemee, lilishe Africa na lilishe Dunia.

(ii) **Mifugo:** Ili kuzalisha mifugo bora inayokidhi mahitaji ya viwanda vya kuchakata nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi, Serikali imeanzisha Vituo Atamizi 8 vya Vijana na wanawake kwa ajili ya mpango wa unenepeshaji wa mifugo katika kampasi za Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) katika kampasi za Buhuri (2), Mabuki (3), Kikulula (2) na vituo vya TALIRI Tanga (1) na Mabuki ambapo kuna vijana wa kike na wa kiume 235. Vijana hao wananenepesha jumla ya ng’ombe 7,050 kwa kila mzunguko mmoja wa unenepeshaji wenye miezi mitatu; kukamilika kwa ujenzi wa majosho 97 na kuendelea na ujenzi wa majosho 160 katika mikoa 25. Ujenzi wa majosho unasaidia kupunguza kundi la jamii za wafugaji ambalo huingia katika umasikini kutokana na kupoteza mifugo yao kwa vifo vitokanavyo na magonjwa yaenezwayo na kupe. Mafanikio mengine ni pamoja na: kuimarisha miundombinu ya masoko ya mifugo na mazao yake; Kuboresha vyuo vya mafunzo ya mifugo; na kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 84,259,375 za chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mifugo. Vilevile, jumla ya michovyo 668,000,278 ya mifugo imefanyika ikiwemo michovyo ya ng’ombe 398,227,019, mbuzi 138,000,211, kondoo 190,207,248 na punda 58,434,200. Udhibiti wa magonjwa ya mifugo utawezesha wafugaji kuwa na mifugo bora na hivyo kupata bei nzuri ya mifugo yao sokoni. Uogeshaji wa mifugo ni muhimu kwa sababu unapunguza matukio ya vifo vya mifugo ambayo kwa asilimia takriban 60 hutokana na magonjwa yaenezwayo na kupe.

Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 imekamilisha ujenzi wa visima viwili (**2**) vya Matanzi (Mkuranga) na Lwami (Mwanga); mabwawa matatu (**3**) ya Kimambi (Liwale), Matekwe (Nachingwea) na Mhanga (Itigi). Aidha, ujenzi wa visima virefu vitatu (**3**) vya Kitaraka (Manyoni), Kapele-kasinde (Momba), Kinamwigulu (Maswa) na mabwawa **11** ya Oloirieni (Ngorongoro), Naalaram (Monduli), Kaiwang (Kiteto), Lerumo (Simanjiro), Kwekikwembe (Kilindi), Msomera (Handeni), Kongwa (Mororogoro DC), Vinyenze (Kibaha), Chang’ombe (Mbeya DC), Kihumbo (Bunda) na Bukabwa (Butiama) unaendelea. Vilevile, katika kuhakikisha upatikanaji wa malisho kwa ajili ya mifugo, Serikali imetambua, kusajili na kutangaza kwenye Gazeti la

Serikali jumla ya hekta 994,827.29 za malisho. Jumla ya shilingi bilioni 15.5 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(iii) **Uvuvi:** Kukamilika kwa ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika kituo cha TAFIRI **-** Dar es Salaam; kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasilimali za uvuvi na mazingira; kujenga na kukarabati miundombinu ya ukuzaji viumbe majini; kuendelea na ujenzi wa mialo ya chifunfu (sengerema) na Igabiro (Bukoba) ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 90; na kuwajengea uwezo wadau 34,195 wa uvuvi kuhusu teknolojia mbalimbali za ufugaji wa samaki na uzalishaji wa vyakula vya samaki. Kadhalika, Serikali imetoa mafunzo kwa vitendo yanayojulikana kama ATAMIZI kwa vijana 200 wanaojishughulisha na uvuvi pamoja na ukuzaji viumbe maji, ili kuzalisha vijana watakaoshiriki katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi na utoaji wa huduma za ugani. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana kujifunza kwa vitendo uvuvi na ukuzaji viumbe maji wenye tija unaoendana na mabadiliko ya teknolojia na uhitaji wa soko na kuongeza fursa za ajira kwa vijana. Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za ununuzi wa boti za uvuvi **118** ikiwa ni awamu ya kwanza ya ununuzi wa boti **160** zilizotarajiwa kununuliwa kwa ajili ya kukopesha wavuvi.

Serikali inatekeleza Mradi wa Nufaika na Ukuzaji Viumbe maji ambapo imekamilisha kuainisha wanufaika wa mikopo ya Pembejeo za ufugaji samaki kwenye vizimba na kilimo cha mwani kupitia mradi wa ECF/IMF. Aidha, Serikali imeingia mkataba na wazabuni sita **(6)** kwa ajili ya kusambaza pembejeo na zana zenye thamani ya shilingi bilioni 14.08 zitakazotolewa kama mikopo ya masharti nafuu isiyo na riba kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa wafugaji samaki **3,154** na wakulima wa mwani **2,030.** Mradi huu utachangia katika kufikia lengo la kuongeza uzalishaji wa samaki wa kufuga kwa mwaka kutoka tani **25,000** hadi tani **50,000,** na mwani kutoka tani **3,500** hadi tani **10,000** kwa mwaka ifikapo mwaka 2025/2026. Kwa upande wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba**, S**erikali imebainisha jumla ya wanufaika **3,154** wa ufugaji samaki kwa njia ya vizimba kati ya hao **91** ni wa vyama vya ushirika na vikundi, makampuni **10** na watu binafsi **32**. Wanufaika hao wanatoka katika halmashauri **19** zinazozunguka ziwa Victoria. Vilevile, hadi kufikia Januari, 2023 vizimba katika Ziwa Victoria vimeongezeka hadi **911** kutoka **653** mwaka 2021/2022**.** Jumla ya shilingi bilioni 6.02 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(iv) **Madini:** Kuanzishwa kwa vituo vipya 26 vya ununuzi wa madini hivyo kufanya vituo vya ununuzi wa madini kuwa 92; kukamilishwa kwa ujenzi wa Vituo vya Umahiri vya Songea, Mpanda na Chunya; kununua madini ya Tanzanite yenye thamani ya shilingi bilioni 2.2; kununuliwa kwa vifaa vya utafiti wa jiosayansi na vifaa vya maabara na uchunguzi katika Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); na kujengewa uwezo kwa watumishi wa Kituo cha Jemolojia Tanzania kuhusu masuala ya uongezaji wa thamani madini; Shirika la Madini la Taifa limenunua mitambo midogo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini; na kununua mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa kwa kutumia makaa ya mawe "*coal briquettes"*. Jumla ya shilingi bilioni 8.36 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

Kutokana na marekebisho ya Sheria ya Madini yaliyoipa GST mamlaka ya kufanya tafiti za kina, GST kwa kushirikiana na Sekta binafsi itafanya tafiti za kina za madini hususan madini ya kimkakati kama vile *nickel, graphite, lithium, copper, rare earth elements na cobalt* ambayo yanahitajika sana katika kutengeneza betri za magari yanayotumia umeme, kompyuta, simu za mkononi, injini za roketi, vifaa vya ndege, brashi za mota za umeme, nyaya za *fibre-optic*, kamera za kidigitali, na vifaa vya kitibabu. Aidha, GST itaongeza kasi ya utafiti wa madini katika maeneo mapya ambayo hayajafanyiwa tafiti na kusogeza huduma za ugani za maabara kwa wachimabji wadogo. Serikali itaanzisha minada ya madini ya Vito *(Gem Auction)* na maonyesho ya madini ya vito *(Gem Fair)* ili kuvutia wanunuzi wakubwa wa madini hayo na kukaribisha waongezaji thamani madini ya vito chini. Aidha, Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) kitaboreshwa kwa kujenga jengo la kisasa la ghorofa 8 ambalo litatumika kutoa mafunzo ya ukataji madini na usonara. Lengo ni kukifanya Kituo hicho kuwa kituo cha uendelezaji madini ya vito nchini.

Kutokana na uwepo wa viwanda vya kusafisha dhahabu nchini *(Refineries)* Serikali itaendelea kuhamasisha madini ya dhahabu yasafishwe kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. Katika kuhakikisha kuwa dhahabu inasafishwa ndani ya nchi, Serikali imepunguza mrabaha kwa wanaouza dhahabu kwenye viwanda hivyo kutoka asilimia 6 hadi asilimia 4. Aidha, Serikali inaziangalia gharama za usafishaji dhahabu ili kumpunguzia mzigo mchimbaji. Vilevile, Benki Kuu ya Tanzania imeanza kununua dhahabu kutoka kwenye masoko ya madini kama inavyoelekezwa kwenye Sheria. Sambamba na hayo, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa madini hasa katika eneo la utoaji leseni, ukaguzi na biashara ya madini. Jumla ya shilingi bilioni 8.36 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(v) **Biashara na Uwekezaji** katika kuchochea biashara na uwekezaji nchini, Serikali imekamilisha utungaji wa Sheria ya Uwekezaji Tanzania namba 10 ya mwaka 2022 na kuendelea kuandaa kanuni zake za Utekezaji. Aidha, wateja 13,836 wamepatiwa huduma katika kituo cha Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (OSC) ambapo miradi 329 (127 wageni, 111 Watanzania, 91 ubia kati ya wageni na Watanzania) ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,517 na inatarajiwa kutoa ajira kwa watanzania wapatao 53,632 nchini. Vilevile, Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji Mahali Pamoja (Tanzania Electronic Investment Window - TeIW) umeweza kuunganishwa (Integrated) na Mifumo kutoka Taasisi za NIDA, TRA, BRELA, TIC, Kazi, Uhamiaji na Ardhi;

(vi) ***Ushirikiano na Sekta Binfsi***, Serikali imeendelea na uratibu wa utekelezaji wa miradi ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi (Public Private Partnership - PPP) inayoibuliwa na Mamlaka za Serikali kwa kuzingatia Sheria ya PPP, Sura 103 na Kanuni zake za mwaka 2020 ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa utaratibu uliozoeleka. Katika mwaka 2023/24, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 10 kupitia PPP Facilitation Fund kwa ajili ya maandalizi ya

maandiko ya miradi ya ubia Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ufanikishaji wa maandalizi ya miradi ya PPP. Miradi hiyo ni kama ilivyoambatishwa katika **Jedwali Na. 1**.

(vii) **Maliasili na Utalii:** kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asimilia 57.7; kuongezeka kwa idadi ya watalii wa ndani kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Ongezeko hili limechangiwa na uhamasishaji kupitia *Royal Tour* iliyoasisiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mafanikio mengine ni kuimarika kwa utalii wa urithi wa utamaduni na malikale; kupungua kwa ujangili na uvunaji haramu wa maliasili; kuongezeka kwa udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu ambapo jumla ya vituo vya askari 16 vimejengwa; kufanya doria za ki-intelijensia na za ushirikiano za kupambana na ujangili katika Kanda 10 za ki-ikolojia za kupambana na ujangili; kukamilika kwa ununuzi na usajili wa viwanda viwili (2) jongea (mobile sawmills) vya kuchakata mazao ya misitu kwa njia endelevu; kusimika mitambo ya kukausha mazao ya misitu kwa kutumia teknolojia ya mionzi ya jua katika wilaya za Liwale na Ruangwa; kununua na kusambaza mizinga 1,013 ya kisasa, jozi 12 za mavazi ya kurinia asali na vifaa vingine vya kuchakata asali katika vijiji 16 vya kongani ya Ruvuma, wilaya za Songea, Mbinga na Nyasa kwa wanufaika vikundi 24; na kupatikana kwa hekta 19.2 za ardhi katika halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Utalii wa Mikutano na Matukio. Jumla ya shilingi bilioni 27.66 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(viii) **Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:** viwanja vilivyopangwa, kupimwa na kuidhinishwa vilikuwa 240,613, sawa na asilimia 83 ya lengo viwanja 291,667 katika kipindi cha hadi Januari 2023. Aidha, lengo kuu ni kupanga, kupima na kuidhinisha viwanja 500,000 kwa mwaka. Matokeo ya ongezeko hili ni pamoja na kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 110 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, sawa na asilimia 94 ya lengo la kipindi hicho la vijiji 117 na asilimia 55.0 ya lengo la mwaka la kupanga vijiji 200. Hivyo, vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya Ardhi vimefikia 2,673 kati ya vijiji 12,318 nchini.

Kupitia Shirika la Nyumba la Taifa, ujenzi wa miradi 8 ya ofisi za Serikali eneo la Mji wa Serikali Mtumba yenye thamani ya shilingi bilioni 186 umefikia wastani wa asilimia 59; mradi wa Morocco Square uliopo jijini Dar Es Salaam wenye thamani ya shilingi bilioni 135 utekelezaji umefikia asilimia 99; na mradi wa Samia Housing Scheme uliopo eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam unaojumuisha majengo 12 yenye nyumba 560 utakaogharimu shilingi bilioni 466 utekelezaji umeanza. Aidha, kupitia jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanyika, Pato la sekta ndogo ya milki (Real Estate) lilikua kwa wastani wa asilimia 4.5 katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2022 kufikia shilingi milioni 1,005,392 ikilinganishwa na shilingi milioni 962,705 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Vilevile, jumla ya miliki 67 (jumla ya ekari 26,263.5) zenye jumla mtaji wa dola za Marekani 2,040,000 zimetolewa kwa wawekezaji;

**B; Miundombinu**

(i) **Reli:** ujenzi wa Reli ya Kati kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 97.91; kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422) asilimia 92.23; Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 25.75; Makutupora – Tabora (km 371) asilimia 4.56; kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi wa kipande cha Tabora - Isaka ( km 163); kupatikana kwa mkandarasi kipande cha Tabora – Kigoma (km 506); na hatua za kumpata mkandarasi kwa kipande cha Uvinza - Malagarasi - Msongati - Gitega(Burundi) - Kindu (DRC) unaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 762.99 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(ii) **Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL):** kufanyika kwa sehemu ya malipo ya ununuzi wa ndege tano (5) ambapo kati ya hizo, ndege moja (1) ni aina ya Boeing 767-300F ya mizigo inayotarajiwa kuwasili Machi 2023, ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 zitakazowasili Julai 2023 na Oktoba 2023, ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner itakayowasili Novemba, 2023 na ndege moja (1) aina ya De Havilland Dash 8-Q400 inatarajiwa kuwasili Juni 2023; ukarabati wa miundombinu katika karakana ya KIMAFA katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA) unaendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Aidha, ununuzi wa vifaa na vipuri kwa ajili ya kuwezesha kufanya matengenezo makubwa na madogo kwa ndege zote unaendelea katika hanga zote za JNIA na KIA; kuanza ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA na ujenzi wa majengo matatu ya kuhifadhia mizigo katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Songwe. Aidha, ATCL imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 14 vya ndani ya nchi pamoja na vituo 10 vya nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 20.52 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(iii) **Viwanja vya Ndege:** kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na barabara za maungio na maegesho ya ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10.2; kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Geita; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Ndege vya Songea (asilimia 98), Iringa (asilimia 42), na Musoma (asilimia 43). Jumla ya shilingi bilioni 41.39 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(iv) **Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Julius Nyerere MW 2,115:** utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 81.86. Aidha, zoezi la ujazaji maji katika bwawa lilizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania tarehe 22 Desemba 2022 ambapo kimo cha maji ya bwawa kimefikia mita 134.39 kutoka usawa wa bahari. Jumla ya shilingi bilioni 869.93 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(v) **Miradi ya Umeme:** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini na vijijini. Sekta hii ni wezeshi katika uzalishaji viwandani, kukuza biashara na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii hivyo kuboresha mazingira wezeshi ya uwekezaji wa sekta binafsi. Hadi Februari 2023 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa ulifikia MW 1,822.05, sawa na ongezeko la asilimia 7.52 ikilinganishwa na MW 1,694.55 zilizokuwepo hadi kufikia Juni 2022. Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ambapo ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze umefikia asilimia 83 na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze umefikia asilimia 48. Aidha, hadi Januari, 2023 jumla ya vijiji 9,467 kati ya vijiji 12,318 vya Tanzania Bara, sawa na asilimia 76.7 vimeunganishwa na huduma ya umeme. Vilevile, mitambo mitatu kati ya minne yenye uwezo wa kuzalisha MW 135 imewashwa kupitia mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I *Extension (MW 185)* na umeme huo kuingizwa katika Gridi ya Taifa. Kadhalika, Serikali imesaini mikataba 26 ya miradi ya kuimarisha Gridi ya Taifa na mikataba 14 ya usambazaji wa umeme vijijini.

(vi) **Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani - Tanga (Tanzania) – EACOP:** kulipwa fidia kwa watanzania 8,386 kati ya 9,508 waliopisha utekelezaji wa mradi; kuendelea na ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa kupasha joto mabomba (thermal insulation plant) katika kijiji cha Sojo, Nzega Tabora ambapo utekelezaji umefikia asilimia 49 ambapo jumla ya shilingi bilioni 30.39 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23. Aidha, Serikali imeendelea kulipia hisa zake katika kampuni ya EACOP kufikia dola za Marekani milioni 131 Januari 2023;

(vii) **Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia – Lindi:** Kuendelea na stadi za kisayansi (geoscience) na stadi za mitambo itakayosimikwa katika eneo la mradi; na kuendelea na majadiliano ya Mkataba wa Nchi Hodhi (HGA) kati ya Serikali na wawekezaji. Jumla ya shilingi milioni 963.0 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(viii) **Ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa:** Kuendelea kuboresha mtandao wa barabara nchini kwa kujenga barabara za mikoa na barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani na barabara za mijini pamoja na ujenzi wa madaraja; kuendelea na ujenzi wa daraja la Kigongo Busisi (Mwanza) pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 63. Jumla ya shilingi bilioni 700.58 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23; Serikali inaendelea na hatua za manunuzi kwa barabara zinazojendwa kwa njia ya PPP na EPC + F kama miradi ilivyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na. 1:**

| Stages | ANNUAL PROCUREMENT PLAN FOR GOODS, WORKS AND NON-CONSULTANCY SERVICES (FOR INTERNAL USE) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sno | Name of Project | Legth (Km) | Approved Budget FY 22/23 (Works +Supervision) in '000,000' Tshs | Estimated Cost at TZS 1.8 Bilion per Km ('000,000 Tshs) | Comments |
| Phase 1 | 1 | Construction of Kibaha - Mlandizi - Chalinze - Morogoro to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 205 | 510 | 738,000 | PPP, Feasibility Study completed for Dar Chalinze, Planned for Chalinze Morogoro |
| | 2 | Construction of Igawa - Songwe - Tunduma to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 218 | 123,707 | 784,800 | |
| Phase 2 | 3 | Construction of Kidatu - Ifakara - Lupiro - Malinyi - Kilosa Mpepo - Londo - Lumechaa/Songea to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 512 | 2,500 | 921,600 | Budgeted for 2023/2024 - Concept Note |
| | 4 | Construction of Arusha - Kibaya - Kongwa Junction to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 453 | 1,100 | 815,400 | |
| | 5 | Construction of Handeni - Kiberashi - Kijingu - Kibaya - Njoro - Olboroti Mrijo Chini - Dalai - Bicha - Chambolo - Chemba - Kwa Mtoro - Singida to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 460 | 3,000 | 828,000 | |
| | 6 | Construction of Masasi - Nachingwea - Liwale to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 175 | 130 | 315,000 | |
| | 7 | Construction of Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 389 | 5,500 | 700,200 | |
| | 8 | Construction of Mafinga - Mtwango to Bitumen Standard By Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F) Mode of Contract | 81 | 291 | 145,800 | |
| | | TOTAL | 2,493 | 136,738 | 5,248,800 | |

(ix) **Barabara na madaraja yanayosimamiwa na TARURA:** Kukamilika kwa matengenezo ya barabara yenye urefu wa km 8,446.78, kati ya hizo km 5,251.23 ni matengenezo ya kawaida, km 1,906.12 matengenezo sehemu korofi na km 1,289.44 ni matengenezo ya muda maalum; kukamilika kwa ujenzi wa bararaba kwa kiwango cha lami zenye urefu wa km 180 na barabara za changarawe zenye urefu wa km 4,785; na ujenzi wa madaraja makubwa na maboksi kalvati 2,368 na mifereji wa maji ya mvua yenye urefu wa km 97.61. Jumla ya shilingi bilioni 343.18 zimetumika katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

(x) **Habari, Mawasiliano na TEHAMA:** kukamilika kwa ujenzi wa njia mpya za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zenye jumla ya Kilometa 1,663; kukamilika kwa ununuzi wa mitambo kwa ajili ya vituo 111 vya kutolea Huduma (transmission and power equipments) ambapo usimikaji umefanyika kwenye vituo 25 vya kutolea huduma za mawasiliano (Point of Presence-POPs and Optical Line Amplifiers OLA) kwenye maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam (1), Pwani (2), Tanga (5), Kilimanjaro (3), Arusha(3), Manyara(2), Morogoro(4), Iringa(2), Dodoma(1), Singida(2); ununuzi wa nguzo (OFC Poles and Accessories) 4,775 zitakazotumika kujenga mkongo wa juu (Overhead Fiber Installation) kwenye maeneo ya njia za Mkongo; kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vya mitambo 39 vya mkongo wa Taifa; na kukamilika kwa ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha mfumo wa kurekodi matukio ya uhalifu wa mtandao. Jumla ya shilingi bilioni 39.6 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(xi) **Uendelezaji wa Bandari:** Kuendelea na uboreshaji wa bandari ya Dar-es-Salaam kwa ujenzi wa gati mpya, upanuzi wa Lango la kuingilia meli na kuongeza kina, Utekelezaji wa Mradi wa kuendeleza miundombinu ya kupokea mafuta (Single Receiving Terminal - SRT) katika Bandari ya DSM, Kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi kuelekea kwenye gati jipya katika Bandari ya Mtwara, Ujenzi wa Gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda lililoko eneo la Chongoleani-Tanga, Kuendelea na mradi wa awamu ya pili ya maboresho katika Bandari ya Tanga, Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo, Ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay, Kupanua Bandari za Lindi na Mtwara, Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA, Kuendelea na ukamilishaji wa miradi ya uboreshaji wa Bandari katika Maziwa, Ujenzi wa kituo cha reli katika Bandari ya Dares salaam, Kununua na kugharamia uhamishaji wa Chuo cha Polisi Kurasini na Kikosi cha Wanamaji (Navy) Kigamboni ili kupisha upanuzi na maendelezo ya shughuli za Bandari. Kuendelea na ununuzi wa mitambo na vifaa vya kupokelea, kupakua na kupakia shehena mbalimbali, Kuendelea na jitihada za kuishirikisha Sekta Binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa Bandari zikiwemo Bandari Kavu ambapo jumla ya shilingi bilioni 242.33 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(xii) **Kuboresha Usafiri wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu:** Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa meli na uboreshaji wa bandari zilizopo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ambapo ujenzi wa meli ya MV. Mwanza umefikia asilimia 82. Jumla ya shilingi bilioni 17.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(xiii) **Uendelezaji wa Viwanda:** Katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, ukarabati wa Kiwanda cha Mashine na Vipuri - KMTC kwa kujenga mtambo wa kuyeyushia chuma umefikia asilimia 98 na kupokelewa kwa kemikali zote nne (4) (Hydrochloric acid lita 4,000, caustic soda kilo 75, zinc ammonium chloride lita 4000 na zinki tani 50) kwa matumizi ya mtambo huo; kuwasili kwa jiko la kuyeyushia chuma (induction furnace) yenye uwezo wa kuyeyusha kilo 500 kwa wakati mmoja ambapo usimikaji umefikia asilimia 60; kukamilika kwa usimikaji wa kreni ya juu (overhead crane) itakayotumika kwenye jiko la kuyeyushia chuma; na kuanza kwa uzalishaji katika kiwanda cha chanjo za wanyama cha Hester Bioscience na kiwanda cha kuunganisha Magari cha GF Trucks Motors ambapo jumla ya magari 595 yameunganishwa. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata ngozi cha Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd (KLICL) umefikia asilimia 45; na kuendelea na ukarabati na ufufuaji wa Kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills Ranch – Morogoro, Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi cha Mamba Ginger Factory Limited na Kiwanda cha Chai cha Mponde – Tanga.

**C; Rasilimali Watu na Huduma za Jamii**

(i) **Elimu:** Kuendelea na utekelezaji wa programu ya Elimumsingi Bila Ada ambapo jumla ya shilingi bilioni 176.1 zimetolewa; kukamilika kwa ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari katika mikoa yote 26; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 657.0 kwa wanafunzi 196,982 wa elimu ya juu; na kuendelea na maboresho ya vyuo ikijumuisha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya shilingi bilioni 1,086.31 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

Katika kuhakikisha kila mtoto anapata fursa ya kusoma, Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha kujengwa kwa Shule mpya 797 za Msingi na 423 za Sekondari ambapo Jumla ya Shilingi bilioni 230.8 zimetumika. Aidha, Serikali imewezesha ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa 27,235 (msingi 5,370 na Sekondari 21,865). Vilevile, Serikali imekarabati Shule kongwe 89 (msingi 48 na Sekondari 41). Pamoja kuongeza upatikanaji wa miundombinu, Serikali katika hicho imeajiri walimu 16,749 (Msingi 9,949 na Sekondari 7,800). Vilevile, idadi ya Shule za Sekondari ya Juu (A- level) zimeongezeka kutoka Shule 810 (436 Serikali na 374 Binafsi) mwaka 2021 hadi kufikia shule 892(509 Serikali na 383 Binafsi) mwaka 2022. Hali kadhalika, ujenzi wa vyuo vipya vya Ufundi Stadi (VETA) unaanza; kimoja cha Mkoa wa Songwe na 64 vya wilaya ambazo hazina vyuo vya VETA. Hii ni sambamba na ukamilishaji wa vyuo vya VETA ngazi za mikoa kwenye mikoa ya Rukwa, Njombe, Geita na Simiyu

(ii) **Afya:** Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa za kikanda na za mikoa; kuendelea na ujenzi wa hospitali 59 za halmashauri na ukarabati wa hospitali kongwe 19 za halmashauri; kuendelea na ukamilishaji wa zahanati 300 katika Halmashauri 184 ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali; kununuliwa na kusambazwa kwa chanjo mbalimbali nchini; kuendelea kutoa huduma za kibingwa na kuanza kutoa huduma za kupunguza uzito kwa kuwekewa puto (Intragastric balloon) kwa wagonjwa 10. Kuendelea kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaatiba na vitendanishi kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma. Aidha, Serikali imenunua mashine za Digital za X – Rays 25; CT – Scan 30, MRI 5 na Mashine za Uchunguzi wa Moyo (7) katika vituo vya kutolea huduma. Vifaa hivi vitasaidia kusogeza huduma za kiuchunguzi karibu na wananchi kwa gharama nafuu hivyo kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa nchini. Kwa mara ya kwanza tangu uhuru wananchi wanaenda kupata huduma za uchunguzi wa magonjwa yao kwa haraka kwa kutumia CT - Scan kuanzia ngazi ya Taifa hadi Mkoa ambapo hapo awali huduma hizi zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya Taifa na baadhi ya Hospitali za Rufaa za Kanda. Jumla ya shilingi bilioni 594.7 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(iii) **Ustawi na Maendeleo ya Jamii:** Kutolewa mkopo kutoka asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri wenye jumla ya shilingi bilioni 28.5 kwa mgawanyo wa vijana (shilingi bilioni 11.7), wanawake (shilingi bilioni 14.1) na watu wenye ulemavu (shilingi bilioni 2.7); Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 463.84 kwa wanawake wajasiriamali; kuendelea kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) na Mkakati wa utekelezaji wake (2005) ambayo ipo katika hatua ya uidhinishaji; kukamilika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na kuandaliwa kwa MTAKUWWA Awamu ya Pili; kukamilika kwa maandalizi ya Programu ya miaka mitano (2022 -2026) ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kwenye Jukwaa la Kimataifa la Kizazi chenye Usawa; kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (Saint John University) na hivyo kufikisha idadi ya madawati 87 ya Jinsia yaliyoanzishwa mpaka sasa katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati; na kufanyika kwa kampeni maalum ya kupinga ukatili dhidi ya watoto hususan ukeketaji katika mikoa yenye matukio mengi ya ukeketaji. Jumla ya shilingi bilioni 2.03 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(iv) **Maji:** Kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ambapo hadi Desemba, 2022 umefikia wastani wa asilimia 77.0 vijijini kutoka asilimia 72.3 Juni, 2021 na mijini asilimia 88.0 kutoka asilimia 86.5 mwaka 2021; Kazi zinazofanyika ni kuendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa miradi 382 kati ya miradi 1,029 iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2022/2023 na kunufaisha wananchi wapatao 2,064,023 kupitia vituo 3,498 vya kuchotea maji vilivyopo katika vijiji 684. Miradi hiyo inahusisha miradi 154 ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa UVIKO – 19, miradi 228 ilitekelezwa kwa fedha za ndani na nje. Baadhi ya miradi ya maji vijijini iliyokamilika ni Mradi wa Maji wa Masoko Group na Mradi wa Maji wa Mwakaleli-I iliyopo katika wilaya ya Rungwe (Mbeya); Mradi wa Maji wa Makongolosi uliopo katika Wilaya ya Chunya (Mbeya); Mradi wa maji wa Mtongwele uliopo katika wilaya ya Newala (Mtwara); Mradi wa maji wa Namanyere ulipo katika Wilaya ya Nkasi na mradi wa maji wa Madaba uliopo Ruvuma (Songea). Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuunda, kuhuisha na kusajili Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs) 82 katika mikoa 25 ya Tanzania bara; na kuajiriwa kwa wataalam 173 kwa mkataba na CBWSOs ambapo kati yao mafundi sanifu ni 144 na wahasibu 29. kukamilisha utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Wanging'ombe; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Mugango – Kiabakari - Butiama ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 71; na kupatikana kwa wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji 28 ambapo wanaendelea na usanifu wa kina wa miradi. Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni kukamilika kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mfumo wa maji katika mji wa Bunda, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya mji wa Mbinga na ujenzi wa mradi wa majisafi wa Kyaka – Bunazi. Jumla ya shilingi bilioni 273.8 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23.

**D; Sekta Mtambuka,**

(i) **Utawala Bora na Usalama wa Raia:** kukamilika na kusainiwa kwa Kanuni za Sheria ya Kuwalinda Mashahidi na Watoa Taarifa za Uhalifu ili zianze kutumika; kuendelea na ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambapo ujenzi wa Ofisi Jumuishi katika Mkoa wa Morogoro umefikia asilimia 53; Mkoa wa Kimashtaka Ilala (Kinyerezi) umefikia asilimia 66.5; Mkoa wa Pwani (asilimia 64.1); Mkoa wa Mbeya (asilimia 54.4); ujenzi wa Ofisi Jumuishi za Huduma za Sheria katika mikoa ya Shinyanga, Manyara, Njombe, Katavi na Sumbawanga umefikia asilimia 15; Kuendelea na ujenzi wa Jengo la makao makuu ya mahakama Jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asimilia 76; Kukamilika na kukabidhiwa kwa Ofisi ya uhamiaji ya Mkoa wa Geita; kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75, Lindi (asilimia 90) na Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Dodoma (asilimia 41); kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Mkuu wa Kikosi cha kutuliza ghasia Singida; na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa kusongeza huduma za mahakama karibu na wananchi na kuongeza idadi ya majaji, mahakimu na mawakili. Jumla ya shilingi bilioni 6.17 zimetumika katika nusu ya kwanza ya mwaka 2022/23;

(ii) **Ajira na Rasilimali watu** katika mwaka 2022/23, Serikali imeendelea kuratibu masuala ya uzalishaji wa fursa za ajira nchini hususan kupitia utekelezaji wa miradi ya kielelezo, uwezeshaji wa mazingira mazuri ya uwekezaji, sambamba na kuimarisha sekta binafsi. Hadi kufikia mwezi Februari 2023, fursa za ajira 547,031 zimezalishwa katika sekta mbalimbali nchini ambapo kati ya ajira hizo, ajira 321,363 zimezalishwa na sekta ya umma ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ajira 225,668 zimezalishwa na sekta binafsi rasmi.

Kwa upande wa rasilimali watu, Serikali inaendelea na programu ya maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya TatuShughuli zitakazotekelezwa ni; Kuwezesha Taasisi za Umma 583 kutekeleza Mifumo ya Usimamizi wa Utendaji kazi ya PEPMIS; kuwezesha utekelezaji wa Mifumo ya HR Assessment na e-HRP; kuwezesha matumizi ya HR Planning na mwongozo wa Urithishaji Madaraka pamoja na HR Development; Mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma; kuanza kwa Ujenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Mbeya; Kuendelea kuongeza uwezo wa kuhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; na kuendelea kuimarisha mifumo na miundombinu ya huduma za Serikali mtandao (e-Governance Services). Jumla ya Shilingi bilioni 11.2 fedha za ndani zimetengwa. Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Taarifa za Kiutumishi n a Malipo ya Mishahara – Home Grown HCMIS, Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na Uboreshaji wa Mfumo wa HCMIS ikiwa ni pamoja na kuanza matumizi ya moduli mpya za Mfumo ikiwemo Watumishi Portal na e-Transfer; kuwajengea uwezo watumiaji; na kuongeza uwezo wa mfumo wa HCMIS kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya Serikali. Aidha, shughuli nyingine ni ujenzi wa Mifumo ya “Optitude Testing” na “Sychometric Testing” ya Sekretarieti ya Ajiras katika Utumishi wa Umma. Jumla ya shilingi bilioni 5.14 fedha za ndani zimetengwa.

(iii) **Ushirikiano wa Kimataifa:** katika kuimarisha mahusiano na nchi za nje na Uchumi wa Kidiplomasia nchini, Serikali imeendelea kuimarisha diplomasia ya kiuchumi hivyo kuwezesha uwekezaji mkubwa kufanyika kupitia usajili wa miradi mbalimbali uliofanywa na Mamlaka ya Eneo Maalumu la Uwekezaji na Mauzo Nje ya nchi (EPZA) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Aidha, ukarabati wa makazi ya balozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji) na nyumba ya mkuu wa utawala Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden) umekamilika na ukarabati wa jengo la ofisi za ubalozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji), makazi ya balozi wa Tanzania Stockholm (Sweden) unaendelea. Vile vile, ukarabati wa majengo nane (8) yanayojumuisha nyumba saba (7) zinazotumika kama kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania Harare (Zimbabwe) umekamilika;

(iv) **Mazingira na Mabadiliko ya Tabia Nchi**: kuandaa mwongozo wa biashara ya hewa ukaa na kanuni zake; kutoa mafunzo ya kuhuisha masuala ya urejeshaji katika mipango, sera na mikakati ya kisekta kwa kikosi kazi cha taifa cha kuhamasisha masuala ya urejeshaji endelevu wa mazingira; kufanya tathmini na kuendeleza utekelezaji wa mipango shirikishi ya usimamizi wa misitu; kuendeleza juhudi za uzalishaji endelevu wa mkaa mbadala na uhamasishaji wa majiko banifu kwa Halmashauri za Wilaya za Kyela, Ludewa, na Makete; na kuwezesha usimamizi endelevu wa rasilimali za maji katika bonde la Ziwa Nyasa;

(v) **Utamaduni, Sanaa na Michezo**: kutoa mikopo kwa wasanii na wadau wa utamaduni 45 yenye thamani shilingi bilioni 1.077; kufanyika kwa maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani katika ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam; timu ya mpira wa miguu kwa wanawake (chini ya umri wa miaka 17), Serengeti Girls, kuweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza ya Tanzania kushiriki katika ngazi ya dunia kwenye soka; na timu ya mpira wa miguu ya watu wenye ulemavu (Tembo Worriors) kufanikiwa kufuzu hatua ya robo fainali na kuiweka nchi kwenye orodha ya timu kumi bora za dunia. Aidha, Serikali imeratibu matamasha mbalimbali yenye lengo la kudumisha urithi wa utamaduni ikiwemo: Tamasha la Utamaduni la Tulia Jijini Mbeya Septemba, 2022; Tamasha kubwa la muziki la CHIGOGO (Cigogo Art and Cultural Festival) wilayani Chamwino; Tamasha la Utamaduni la Maasai Jijini Arusha Oktoba, 2022 kwa kushirikisha zaidi ya vikundi vya utamaduni 72; Tamasha la tano (5) la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki, (JAMAFEST) lililofanyika Septemba, 2022 Jijini Bujumbura, Burundi; Tamasha la 41 la Kimataifa la Utamaduni na Sanaa la Bagamoyo; na Tamasha la Msimu wa Utamaduni kati ya Tanzania na Afrika Kusini mwezi Novemba 2022. Vilevile, timu za Simba na Yanga zimenufaika na ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kununua kila goli kwa michezo ya kimataifa inayochezwa ambapo hadi sasa timu ya Yanga imepata shilingi milioni 25 na Simba shilingi milioni 10. Hatua hii imeongea hamasa kwa timu za Tanzania kushiriki katika mashindano ya kimataifa;

(vi) **Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP):** katika mwaka 2022/2023 Serikali imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali kuhusu Programu ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kama yafuatayo: Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Kituo cha PPP ili kiweze kuanza utekelezaji wa majukumu yake; ukamilishaji wa taarifa ya Upembuzi Yakinifu wa miradi mitatu (3) inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Miradi hiyo ni pamoja na - Mradi ya ujenzi wa Mabweni katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kampasi ya Dar es Salaam, Mradi wa Ukaguzi wa Lazima kwa Vyombo vya Moto Nchini kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Mradi wa Kuimarisha Huduma za Saratani nchini jijini Dar es Salaam na Mbeya kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI); kupatikana kwa mbia mpya wa uendeshaji wa mradi wa BRT, ujenzi wa majengo ya biashara na hoteli ya nyota nne katika kiwanja cha ndege cha JKN, Mafanikio mengine ni Kufanya mapitio ya Sheria ya PPP, Sura 103 ambapo wadau kutoka Sekta ya Umma, Sekta Binafsi, na Washirika wa Maendeleo walishirikishwa kuandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya PPP. Aidha, Muswada wa marekebisho ya Sheria ya PPP wa mwaka 2023 umekamilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge la mwezi Februari, 2023;

(vii) **Ushiriki wa Sekta Binafsi**: Ushiriki wa sekta binafsi umeendelea kuongezeka ambapo jumla ya miradi 329 (127 wageni, 111 Watanzania na 91 ubia kati ya wageni na Watanzania) ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,517 na inatarajiwa kutoa ajira kwa watanzania wapatao 53,632. Aidha, katika azma ya Serikali kuendelea kuishirikisha na kuiwezesha sekta binafsi katika shughuli za kiuchumi, miradi na huduma nyingi zilitolewa na sekta binafsi kupitia bajeti ya Serikali. Kutokana na kuendelea kujenga mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji pamoja na ushirikiano na sekta binafsi, matokeo chanya yameanza kupatikana kwa kuongezeka uzalishaji viwandani ambavyo pia vimeongeza thamani ya mazao ya kilimo pamoja na ajira. Aidha, kiwanda cha sukari cha Bagamoyo kimeanza uzalishaji kwa wastani wa tani 25,000 kwa mwaka na hivyo kupunguza pengo la mahitaji ya ndani; na

(viii) **Sensa ya watu na Makazi:** kukamilika kwa zoezi la sensa ya watu, makazi na majengo na kuzinduliwa matokeo yake na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 31 Oktoba, 2022. Aidha, matokeo hayo yamebainisha kuwa idadi ya watu nchini imefikia watu 61,741,120 kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012.

## B. MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24

12. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayotekelezwa kupitia Mpango Elekezi wa Muda Mrefu, 2011/12 - 2025/26 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 wenye dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Maandalizi ya Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Mwaka 2023/24 yamezingatia nyaraka za kisera za kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

13. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** Mapendekezo ya Serikali ya Mpango yameainisha malengo na shabaha za Serikali katika kuimarisha uchumi. Aidha, Mpango umeainisha miradi na programu za maendeleo mahsusi kwa ajili ya kufikia malengo na shabaha hizo ambapo kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hiyo ndio msingi na nyenzo muhimu katika kujenga uchumi shindani na wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Aidha, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa miradi ya kielelezo na kimkakati inayotarajiwa kuwa na matokeo mapana na ya haraka katika uchumi. Miradi hiyo inajumuisha: ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge); kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115; kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) - Lindi; makaa ya Mawe (Mchuchuma - Njombe) na Chuma (Liganga - Njombe); na kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) - Njombe. Vilevile, Serikali itafanya maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za mitaa wa mwaka 2024 na uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 pamoja na maandalizi ya Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050. Kadhalika Serikali itaendelea: kutekeleza diplomasia ya uchumi; kuimarisha mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kutekeleza wa mkakati wa uchumi wa buluu.

14. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** Miradi ya kipaumbele **kwa mwaka 2023/24** itazingatia maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Miradi itakayotekelezwa itajikita katika maeneo yafuatayo:

(i) **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi**: miradi itakayotekelezwa itajumuisha ujenzi na ukarabati wa reli ya kati iliyopo; ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi na zile za kuunganisha Tanzania na nchi jirani; ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu; kuboresha Bandari za Dar es Salaam na Tanga; ujenzi wa viwanja vya ndege; miradi ya kufua umeme; na kusambaza umeme vijijini;

(ii) **Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma**: miradi itakayotekelezwa itajumuisha uendelezaji wa Viwanda Vidogo - SIDO, ujenzi wa bandari ya Uvuvi, Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II; upatikanaji wa mbegu bora Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji; kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo; kuwezesha Uongezaji Thamani Mazao ya Mifugo; na ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO). Aidha, Serikali imeanza uwekezaji wa muda mrefu katika sekta ya kilimo kwa kuendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II. Utekelezaji huo unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao hasa ya chakula ili kujihakikishia usalama wa chakula kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya watu linalotazamiwa kufika milioni 80 mwaka 2050 kutoka Milioni 61.7 za sasa. Aidha, ongezeko la uzalishaji litawezesha kupata akiba itakayouzwa nje ya nchi na hivyo kuwezesha nchi kupata mapato ya kigeni na kupunguza urari hasi wa biashara.

Ili kufikia malengo hayo, sekta ya kilimo itatekeleza vipaumbele vifuatavyo: Kuongeza uzalishaji kwa tija kwa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, utafiti wa mbegu, upatikanaji wa mbegu bora na kuimarisha huduma za ugani na kuongeza upatikanaji wa mbolea ya ruzuku na viuatilifu; Kuongeza usalama wa chakula kwa kuimarisha miundombinu ya uhifadhi ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kuongeza uwezo wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) wa kuhifadhi mazao kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000 na kuhakikisha NFRA inanunua na kuhifadhi chakula cha kutosheleza Taifa kwa muda wa miezi sita (6); Kuimarisha kilimo cha mashamba makubwa (Block farms); na kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao;

(iii) **Kukuza Biashara na Uwekezaji:** miradi itakayotekelezwa itajielekeza katika kuratibu, kuhamasisha, kutangaza na kuwezesha uwekezaji, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi;

(iv) **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** miradi itakayotekelezwa itajielekeza katika kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma zitakazotolewa katika sekta za huduma za jamii zikiwemo afya, elimu na maji; na

(v) **Kuendeleza Rasilimali Watu:** miradi itakayotekelezwa inajumuisha Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini; Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha; na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

## SEHEMU YA TATU

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI JANUARI 2023 NA MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24

### A. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI JANUARI 2023

15. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika mwaka 2022/23, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 41,480.6. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 26,474.6 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 15,006.0 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

16. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, Serikali ilitarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 24,122.5. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 22,236.7 kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 92.2 ya lengo. Mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 15,625.3, sawa na asilimia 97.1 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 16,084.9. Kati ya mapato ya ndani, mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi bilioni 13,601.2, mapato kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea na gawio kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma shilingi bilioni 1,461.4 na mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa shilingi bilioni 562.6.

17. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kufikia malengo yaliyowekwa. Baadhi ya hatua za muda mfupi zinazoendelea kuchukuliwa ni pamoja na: kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka yote nchini kwa kufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti ukwepaji kodi na biashara za magendo; kuendelea kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA (EFDMS, TANCIS, ITAX) kwa ajili ya kufuatilia kiasi cha fedha kinachopaswa kulipwa na walipakodi; kuendelea na kampeni mbalimbali nchini za kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia semina, makongamano na vyombo vya habari kwa lengo la kupata maoni juu ya njia bora ya kuwahudumia ili kuongeza uhiari wa kulipa kodi; kuendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali; kuhimiza matumizi ya mfumo huo ili kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali; na kuendelea kufanya ufuatiliaji wa vyanzo vinavyokusanya mapato yasiyo ya kodi.

18. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023, shilingi bilioni 3,087.4 zimepokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 90.6 ya lengo la shilingi bilioni 3,407.1. Kati ya kiasi kilichotolewa, misaada na mikopo nafuu ya kibajeti (GBS) ilikuwa shilingi bilioni 1,498.5, sawa na asilimia 91.5 ya lengo, misaada na mikopo nafuu ya mifuko ya pamoja ya kisekta ni shilingi bilioni 64.1, sawa na asilimia 58.6 ya lengo, na misaada na mikopo nafuu ya miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,524.7, sawa na asilimia 91.8. ya lengo la kipindi cha marejeo.

19. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Januari 2023 Serikali ilikopa katika soko la ndani kiasi cha shilingi bilioni 2,971.9, sawa na asilimia 91.2 ya kiasi kilichopangwa kukopwa cha shilingi bilioni 3,260.0 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi kilichokopwa, shilingi bilioni 2,117.0 zilitumika kulipia hatifungani zilizoiva na shilingi bilioni 854.9 zilitumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, hadi Januari 2023, Serikali ilifanikiwa kukopa shilingi bilioni 552.3 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara**.**

20. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** kwa upande wa matumizi, ridhaa ya matumizi iliyotolewa katika kipindi kilichoishia Januari 2023 ilikuwa shilingi bilioni 23,272.5, sawa na asilimia 96.5 ya lengo. Kati ya kiasi kilichotolewa, shilingi bilioni 14,635.8 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 95.7 ya lengo na shilingi bilioni 8,636.7 ni fedha za maendeleo, sawa na asilimia 97.8. Aidha, matumizi zaidi ya mapato halisi ya shilingi bilioni 1,035.8 yaligharamiwa na mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

21. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika kipindi cha Machi hadi Juni 2023, Serikali itaendelea kupeleka fedha kwenye mafungu kwa kuwianisha mapato na matumizi, na kwa kuzingatia ukomo wa kila fungu. Maeneo muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na: Ugharamiaji wa deni la Serikali, ulipaji wa mishahara ya watumishi, ugharamiaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na Elimumsingi Bila Ada, uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati, ikijumuisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, ujenzi wa mradi wa kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere. **Maelezo ya kina yanapatikana katika Kiambatisho cha Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti kwa Mwaka 2023/24.**

## B. MAPENDEKEZO YA MFUMO NA UKOMO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2023/24

### Sera za Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2023/24

22. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** sera za mapato na hatua za kiutawala kwa mwaka 2023/24 zitalenga kuongeza makusanyo ya mapato kwa kuendelea kutekeleza yafuatayo: Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini katika sekta za uzalishaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi; kuongeza wigo wa mapato; kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato ya ndani; kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za kodi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuongeza uwekezaji ili kuongeza mapato; kudhibiti misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja (1) ya Pato la Taifa; kufanya tafiti na tathmini zinazolenga kuibua fursa mpya za mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; na kuendelea kuimarisha mifumo ya Mashirika, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa Mfuko Mkuu kwa wakati.

23. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** katika mwaka 2023/24, Serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Lengo kuu ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, na kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kugharamia mahitaji yasiyoepukika ikijumuisha mishahara na deni la Taifa. Aidha, Serikali itaendelea kugharamia miradi ya maendeleo inayochochea ukuaji wa uchumi, kuboresha huduma za jamii, kuongeza uzalishaji na mauzo nje pamoja na maeneo yenye vyanzo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo maalum yenye maslahi mapana kwa Taifa kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Maji na Wakala wa Maji Vijijini. Vilevile, Serikali itaendelea kudhibiti ongezeko la malimbikizo ya madai, madeni pamoja na kufanya maboresho katika mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma ili kuongeza tija, ufanisi na thamani ya fedha katika ununuzi wa umma.

**MFUMO NA UKOMO WA BAJETI KWA MWAKA 2023/24**

24. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** uandaaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023/24 pamoja na Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha mwaka 2023/24 umejengwa katika shabaha na misingi (*assumptions*) ifuatayo:

**Shabaha na malengo ya uchumi jumla**:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 2022;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 14.9 ya Pato la Taifa mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23 kutoka matarajio ya asilimia 11.5 mwaka 2022/23;

(v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**Misingi:**

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili, yasiyo ya asili na mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Kuendelea kuhimili athari zitokanazo na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia na kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la dunia;

(iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

25. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*,** Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali ikiwemo: Mfumuko wa bei; viwango vya kubadilisha fedha; ukuaji wa Pato la Taifa; viwango vya riba katika soko la fedha la ndani na nje; mabadiliko ya tabianchi (ukame/mafuriko) na uharibifu wa mazingira; majanga asilia kama vile matetemeko ya ardhi na magonjwa ya mlipuko; mabadiliko ya sera za ufadhili za misaada za Washirika wa Maendeleo kwa nchi zinazoendelea; ubadhirifu wa fedha na mali za umma; na madeni sanjari (contingent liabilities). Athari zinazoweza kujitokeza endapo vihatarishi vya mwenendo wa uchumi jumla na utekelezaji wa bajeti vitatokea ni pamoja na: kuongezeka kwa nakisi ya bajeti; kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato; kupungua kwa uzalishaji viwandani na mashambani; kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za maisha kwa wananchi na utekelezaji wa miradi; kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni la Serikali; kuongezeka kwa gharama za mikopo ya kibiashara katika masoko ya fedha; kupungua kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo; kuongezeka kwa madai na madeni ya wazabuni na watoa huduma; na kuongezeka kwa Deni la Serikali.

26. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, mikakati ya kukabiliana na vihatarishi ni pamoja na: kusimamia miongozo ya kubaini vihatarishi katika uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ili kuchukua hatua stahiki za kisera na kiutawala kabla, wakati na baada ya kutokea; kuimarisha uwezo wa Serikali katika kupambana na vitendo vya ukwepaji kodi ikiwemo uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA, udhibiti wa biashara za magendo, utoaji wa elimu kwa mlipakodi pamoja na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato; kutoa unafuu wa upatikanaji wa pembejeo ikiwemo mbolea, zana za kilimo, viuatilifu, mbegu bora na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

27. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*,** kwa kuzingatia sera za bajeti kwa mwaka 2023/24, Sura ya Bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 44,388.1 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho, sawa na ongezeko la asilimia 7.0 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ya mwaka 2022/23 ya shilingi bilioni 41,480.6. Jumla ya mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 31,381.0, sawa na asilimia 70.7 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 13.0 hadi shilingi bilioni 26,725.4 kutoka makadirio ya shilingi bilioni 23,652.8 mwaka 2022/23. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 5,466.2, sawa na asilimia 12.3 ya bajeti yote. Aidha, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 5,440.4 kutoka soko la ndani ambapo shilingi bilioni 3,542.1 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi bilioni 1,898.3 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 2,100.5 kutoka soko la nje kwa masharti ya kibiashara ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

28. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika mwaka 2023/24, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 44,388.1 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 29,232.1 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha shilingi bilioni 12,771.5 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za Mfuko Mkuu na shilingi bilioni 10,882.1 kwa ajili ya mishahara ikiwemo upandishaji wa madaraja kwa watumishi na ajira mpya, na shilingi bilioni 6,396.9 kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC). Matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 15,156.0. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 11,873.9 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 78.3 ya bajeti ya maendeleo na shilingi bilioni 3,282.1 ni fedha za nje. Ukomo wa fedha za maendeleo upo ndani ya wigo wa kati ya asilimia 30 na 40 ulioanishwa kwenye Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26). Utengaji wa fedha za maendeleo umezingatia miradi inayoendelea ikiwemo miradi ya kimkakati na ya kielelezo pamoja na utekelezaji wa miradi kupitia utaratibu wa PPP ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa utaratibu uliozoeleka. Aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kufuatia kukamilika kwa miradi ya maendeleo hususan kwenye sekta za huduma za jamii ambazo kwa sasa zinahitaji fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya uendeshaji.

29. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa kuzingatia maelezo hayo, mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti kwa mwaka 2023/24 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2**:

**Jedwali Na.2: Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24**

| | | | | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mapato | 2022/23 | 2023/24 | Ongezeko/ Upungufu | Ongezeko /Upungufu (Asilimia) |
| A. | **Mapato ya Ndani-Serikali Kuu** | **27,005,581** | **30,237,128** | **3,231,547** | **12.0%** |
| | (i) Mapato ya Kodi na yasiyo ya kodi (TRA) | *23,652,758* | *26,725,409* | **3,072,651** | **13.0%** |
| | (ii) Mapato yasiyo ya kodi | *3,352,824* | *3,511,719* | **158,896** | **4.7%** |
| B. | **Mapato ya Halmashauri** | **1,012,286** | **1,143,883** | **131,597** | **13.0%** |
| C. | **Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo** | **4,648,561** | **5,466,215** | **817,654** | **17.6%** |
| | (i) Misaada na Mikopo nafuu - GBS | *1,949,480* | *2,184,134* | **234,654** | **12.0%** |
| | (ii)Misaada na Mikopo nafuu ya Miradi | *2,576,958* | *3,151,958* | **575,000** | **22.3%** |
| | (iii)Misaada na Mikopo nafuu ya Kisekta | *122,123* | *130,123* | **8,000** | **6.6%** |
| D. | **Mikopo ya Ndani na Nje** | **8,814,152** | **7,540,840** | **-1,273,311** | **-14.4%** |
| | (i) Mikopo ya Nje | *3,034,004* | *2,100,464* | **-933,540** | **-30.8%** |
| | (ii) Mikopo ya Ndani | *2,480,148* | *1,898,316* | **-581,832** | **-23.5%** |
| | (iii)Mikopo ya Ndani- Rollover | *3,300,000* | *3,542,061* | **242,061** | **7.3%** |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE (A+B+C+D)** | **41,480,580** | **44,388,067** | **2,907,487** | **7.0%** |
| | | | | | |
| | **Matumizi** | | | | |
| E. | **Matumizi ya Kawaida** | **26,474,578** | **29,232,092** | **2,757,514** | **10.4%** |
| | | | | | |
| | o/w (i) Mfuko Mkuu wa Serikali | **11,308,364** | **12,771,533** | **1,463,169** | **12.9%** |
| | -Malipo ya Riba Ndani | *1,770,159* | *2,799,374* | **1,029,215** | **58.1%** |
| | -Malipo ya Mtaji Ndani (Rollover) | *3,300,000* | *3,542,061* | **242,061** | **7.3%** |
| | -Malipo ya Mtaji Nje | *2,916,041* | *2,763,947* | **-152,095** | **-5.2%** |
| | - Malipo ya Riba Nje | *1,100,802* | *1,364,377* | **263,575** | **23.9%** |
| | - Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii | *1,655,652* | *1,710,608* | **54,955** | **3.3%** |
| | -Matumizi Mengine ya Mfuko Mkuu | *565,710* | *591,167* | **25,457** | **4.5%** |
| | (ii) Mishahara | ***9,830,753*** | ***10,882,126*** | **1,051,373** | **10.7%** |
| | (iii)Matumizi Mengineyo (OC) | ***5,335,461*** | ***5,578,433*** | **242,972** | **4.6%** |
| | - Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *200,000* | *200,000* | **0** | **0.0%** |
| | - Matumizi ya Halmashauri (own source) | *617,485* | *749,083* | **131,597** | **21.3%** |
| | - Matumizi mengineyo | 4,517,976 | 4,629,351 | **111,375** | **2.5%** |
| F. | **Matumizi ya Maendeleo** | **15,006,002** | **15,155,975** | **149,973** | **1.0%** |
| | (i) Fedha za Ndani | *12,306,921* | *11,873,894* | **-433,027** | **-3.5%** |
| | o/w Malipo ya Madeni yaliyohakikiwa | *230,000* | *528,000* | **298,000** | **129.6%** |
| | o/w Ugharamiaji wa SGR | *1,113,000* | *1,500,000* | **387,000** | **34.8%** |
| | o/w Ugharamiaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere | *1,435,000* | *1,450,000* | **15,000** | **1.0%** |
| | o/w Matumizi ya Halmashauri (own Source) | *394,801* | *394,801* | **0** | **0.0%** |
| | o/w Miradi mingine | *9,134,120* | *8,001,093* | **-1,133,027** | **-12.4%** |
| | (ii) Fedha za Nje | *2,699,081* | *3,282,081* | **583,000** | **21.6%** |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE (E+F)** | **41,480,580** | **44,388,067** | **2,907,487** | **7.0%** |
| | **NAKISI YA BAJETI (ASILIMIA YA PATO LA TAIFA)** | **3.3%** | **2.7%** | | |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**HITIMISHO**

30. ***Mheshimiwa Mwenyekiti***; Katika mwaka 2023/24, Serikali inatarajia kuongeza ukusanyaji wa mapato, ili kugharamia sehemu kubwa ya matumizi yake na kuendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 pamoja na sheria nyingine kwa lengo la kubana matumizi na kuelekeza fedha kwenye utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa.

31. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 pamoja na Mfumo na Ukomo na Bajeti ya mwaka 2023/24, unatarajiwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kuimarisha sekta za uzalishaji ili kutoa mchango zaidi katika ukuaji wa uchumi, kuongeza mapato ya Serikali, fursa za ajira na maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla na kuongeza upatikanaji wa huduma bora za kijamii kama vile elimu, afya, maji, barabara n.k.

32. ***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** naomba kuwasilisha.